OFISI YA RAIS ,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA SENGEREMA
SHULE YA SEKONDARI SENGEREMA

S.L.P 42
SENGEREMA

10/06/2017
SIMU: 0282590088

Mzazi wa :…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii mwaka 2017. Anapaswa kufika shuleni tarehe **16/07/2017** kabla ya saa 11.00 jioni . Shule ipo kata ya **Mwabaluhi** Wilaya ya Sengerema-Mwanza umbali wa kilometa 1.3 kutoka stendi kuu ya mjini Sengerema . Anaweza kufika shuleni kwa teksi Tsh 3000/= au pikipiki kwa Tsh 1000/=

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.0 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

1.1 **Ada ya shule** ni Tshs. 70,000/= kwa mwaka.

Fedha za ada zilipwe kwenye akaunti Na. **31601200040 NMB tawi lolote Tanzania**. Jina la akaunti hiyo ni **Sengerema Secondary School Recurrent Account.**.

1.2 **Michango ya Shule**.

Fedha za michango ya Shule` zilipwe kwenye akaunti Na. **31601100001 NMB tawi lolote Tanzania**. Jina **Sengerema Secondary School Fund Account**.

Tahadhari (hazitarudishwa)	5,000/=
Taaluma	20,000/=
Matibabu	10,000/=
Kitambulisho, picha na nembo	8,000/= (**atalipia Shuleni**)
Ukarabati wa Samani	15,000/=
Wapishi,walinzi na vibarua wengine	30,000/=
Uendeshaji wa Mitihani	20,000/=
Jumla	**108,000/=**

2.1."Shule haipokei fedha taslimu".Fedha zote zilipwe kupitia Benki ya NMB tawi lolote, kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi za malipo (**Bank pay in slips**) zenye jina la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti**. Mwanafunzi hatapokelewa shuleni endapo hatakamilisha malipo yote ya fedha kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu.**

2.2. Tarehe ya kufungua shule imeoneshwa hapo juu, mwanao akichelewa kuripoti shuleni ndani ya **siku kumi na nne atakuwa** amepoteza nafasi yake.

2.3. Aje na photocopy ya nakala halisi ya uraia au cheti cha kuzaliwa na **result slip** ya matokeo ya kidato cha **NNE**

2.4 Mwanafunzi na mzazi/mlezi wakumbuke kusoma kwa makini/kujaza na kusaini fomu ya sheria za shule na kukiri kusoma kwa bidii na kufaulu mitihani yetu na fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano endapo kutatokea dhalura.

2.5 Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi iliyojazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali iwasilishwe siku ya kuripoti shuleni.
2.6. Nguo za nyumbani haziruhusiwi, mwanafunzi atavaa sare za shule muda wote awapo shuleni. Pindi anapokuja shuleni kuripoti awe amevaa suruali nyeusi ya kitambaa na shati nyeupe yenye mikono **mirefu isiyokuwa na vishikizo vya chuma.**
2.7.Kila mzazi /mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanae kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo na kumpa fedha kwa ajili ya matumizi yake binafsi. Mzazi kumbuka kuwa kumpa mwanao fedha kupita kiasi kunaweza kuchangia kuporomoka kwa elimu yake.

3.0 SARE YA SHULE
3.1 Suruali mbili nyeusi za kitambaa zenye malinda mawili kwa mbele na mfuko mmoja nyuma.
3.2 T-shirt mbili rangi ya bluu bahari yenye kola nyeusi kwa matumizi baada ya vipindi vya darasani.
3.3 Sweta rangi ya dark bluu.
3.4. Tai rangi ya dark bluu
3.5. Tshirt ya michezo rangi ya kijivu isiyo na kola..
3.6 Shati mbili nyeupe za mikono mirefu na ziwe na vishikizo vya kawaida na si vya chuma.
3.7 Soksi nyeupe jozi mbili.
3.8 Viatu vya kufunika vyeusi vya ngozi jozi mbili visivyo vya kuchongoka kwa mbele na viwe na visigino vifupi.

4.0 MAHITAJI MENGINE
4.1 Godoro 3" x 2.5 x 6". Vitanda vya shule vina ukubwa huo.
4.2 Ream za karatasi mbili (2) **Double A**
4.3 Bukta rangi ya bluu moja.
4.4 Raba za michezo pea moja.
4.5 Shuka 2 rangi ya bluu bahari.
4.6 Mto na foronya
4.7 Ndoo 1, dumu 1 kubwa, na dumu 1 dogo kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa kijiko,sahani ya shaba,bakuli la shaba na kikombe kwa ajili ya uji.
4.8 Taa ya betri kwa tahadhali ya umeme ukikatika (**ISIWE YA KUCHAJI**). **Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakuja na taa hiyo.**
4.9 Madaftari makubwa (counter books) angalau kumi(10) au zaidi
4.10 Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi .
4.11 Flat file rangi ya pink au blue kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi (file lisiwe la spring)
4.12 Blanketi la kujifunika na neti ya Mbu rangi ya light bluu.
4.13 Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
4.14 Vitabu vyake binafsi vya kujisomea.
4.15 Sanduku la chuma.

5.0 VIFAA VYA USAFI
5.1 Soft broom 1
5.2 Fyekeo 1 au reki 01
5.3 Chelewa ndefu ya nje (fagio la wima) 1
5.4 Squeezer moja (mpira wa kukaushia maji) 1 au Jembe lenye mpini mmoja

N:B Vifaa vilivyoorodheshwa hapo juu pia vinapatikana katika duka lililoko Shuleni kwa wale wanaotoka mbali na watakaokosa baadhi ya vifaa.

KARIBU SANA

"ELIMU NI DHAMANA"

Z.L. KAHEMA
MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS ,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI SENGEREMA
S.L.P. 42, SENGEREMA MWANZA Simu 028-2590088

HATI ZA SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anayejiunga na Shule hii anatakiwa kuzisoma vizuri kisha atasaini pamoja na Mzazi au Mlezi wake Wakati wa kuripoti atarudisha hati hii shuleni.

Mwanafunzi awapo Shuleni anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kusoma kwa bidii na kuzingatia masomo yake kwa umakini .**Kila mwisho wa mhula,Mwanafunzi atapewa matokeo yake ya mhula mkononi,Mzazi/Mlezi** hakikisha unayapata na mwanao asipofikisha wastani uliowekwa na Shule Mzazi/Mlezi utatakiwa kufika Shuleni kwa ajili ya kujadili maendeleo ya taaluma ya mwananafunzi kwa kushirikiana na Uongozi wa Shule.
2. Heshima miongoni mwa wanafunzi na kuwaheshimu Walimu, Walezi na Jumuiya nzima ya Shule na Jamii inayoizunguka shule.
3. Kulinda na kutunza mazingira ya Shule na mali ya Shule na kuhakikisha unafanya USAFI katika maeneo utakayopangiwa na viongozi wako..
4. Kuzingatia ratiba ya Shule darasani ,bwaloni, usafi, mradi, bwenini na paredi..
5. Huruhusiwi kwenda nyumbani kwa Walimu bila idhini..
6. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza. Kila mwanafunzi ajitahidi kujifunza kwa bidii na kujizoesha kuongea Kiingereza.
7. Mgeni atakaye kutembelea sharti apate kibali kutoka Uongozi wa Shule. Ni marufuku kumtembeza mgeni yeyote katika maeneo ya Shule bila kibali cha Uongozi wa Shule.
8. Mawasiliano yote yapitie kwa Walezi. **Mwanafunzi HARUHUSIWI <u>kuwa na simu ya mkononi.</u>**
9. Kutotoa lugha chafu kwa walezi wote.
10. Kutovaa mavazi ya kihuni, Mavazi yanayoruhusiwa Shuleni ni mashati meupe yenye mikono mirefu yatakayokuwa na nembo ya Shule na T-shirt zenye nembo ya Shule na suruali nyeusi tu.
11. Nywele zisizozidi 0.5 cm na ndevu zinyolewe wakati wote.

MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uvutaji wa bangi, sigara na madawa ya kulevya.
3. Makosa ya jinai.
4. Kupigana, kupiga au kuchochea ugomvi.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma au Jamii inayozunguka Shule.
6. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo waTaifa.
7. Kuoa.
8. Kumpa msichana mimba au kusaidia kutoa mimba.
9. Kuanzisha, kuchochea na kushiriki mgomo.
10. Kuwa mtoro wa vipindi au kuzurura mjini.
11. Kuonekana kwenye nyumba za starehe na kumbi za starehe, mfano nyumba ya kulala wageni n.k.
12. Kuwa na simu ya mkononi.
13. Kuwa na pasi ya umeme, jiko na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha ajali ya moto.

Kama kuna tatizo lolote, mawasiliano yafanyike kupitia kwa Viongozi wa Wanafunzi, Mwalimu wa Zamu, Nyumba, Madarasa na Uongozi wa Shule ili kuepusha migogoro Shuleni.

Mimi ……chaguo……. .nakubali kutii sheria na maagizo haya ya Shule. Pindi nitakapovunja sheria na maagizo haya, hatua kali zichukuliwe kulingana na sheria na taratibu za Shule.

Jina na Sahihi ya Mzaz iau Mlezi ……. Tarehe ……

SENGEREMA DISTRICT COUNCIL
SENGEREMA SECONDARY SCHOOL
REQUIREST FOR MEDICAL EXAMINATION

From the Headmaster
Sengerema Secondary School
P.O.Box 42
SENGEREMA

To the Medical Officer.....(Name in full)

Please examine the above named student as to his physical and mental fitness for a full time student. The examination should oinclude the following categories (a-c).

(a) (i) Eyesight (ii) Hearing (iii) speech (iv) limbs (v) general diseases (vi) leprosy (vii) epilepsy
(b) Neurosis
(c) Other series diseases e.g Asthma, TB etc.

Name .....date.....sgnature.....

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(i) Eyesight .....

(ii) Hearing .....

(iii) Speech.....

(iv) Limbs .....

(v) General diseases .....

(vi) Leprosy.....

(vii) Epilepsy.....

(viii) Neurosis.....

(ix) Other series diseases e.g Asthma,.....

(x) TB etc.....

Comment.....
.....
Name .....date.....sgnature.....

STATION .....DESIGNATION.....

MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA

Ili mwanafunzi aweze kupata elimu bora na yenye kumwezesha kukabiliana na mazingira halisi, anapaswa kuwa na vitabu. Hivi hapa ni baadhi ya vitabu ambavyo anapaswa kuja navyo ili aweze kumudu sawasawa mchepuo wake:

1. KISWAHILI
    - Kiswahili Sekondari – Taasisi ya elimu
    - Sarufi na Fasihi- Sekondari na Vyuo (Felician Nkwera)
    - Nadhalia ya Lugha – Chaja Masebo na N.Nyangwine
    - Tafsiri na Ukalimani – Wanjara
    - Nadhatia ya Fasihi – J.A. Masebo
2. HISTORY
    - Mastering Advanced Level History book I and II – Kato (2010)
    - Basic Themes in European Advanced level history paper I and II (Ismail Ngobi-2012)
    - Major Events in Africa History paper I (FR. Jovitus F. Kamara)
3. ENGLISH LANGUAGE
    - Advanced Literature
    - Advanced level literature an essential guide – Nicholaus Asheri
    - A man of the people by Chinua Achebe

4. COMMERCE
    - Textbook of Commerce – By Dinah
    - Essenmtial Commerce for East Africa
    - Advanced level Commerce
    - Commerce simplified
5. GEOGRAPHY
    - General geography in Diagrams (R.E Bunnett)
    - Practical Geography for Africa (John M. Pritchard)
    - Physical Geography for Africa (D.T Msabila)
    - Human and Economic Geography (D.T Msabila)
6. PHYSICS
    - S. Chand's Principle of Physics – Class XI & XII -
    - Principle of Physics – Rogers Municaster
    - Advanced Level Physics – Nelkon & Parlker
    - Principles of Physics – Tom Duncan
7. BIOLOGY
    - Advanced Biology for Secondary schools - (Michael R.)
    - Biological Science – (Taylor O J & Stoud G.W)
    - Cell structure and Organization – L. Msaki
    - Understanding Biology – Fourth edition
8. ADVANCED MATHEMATICS
    - Advanced Level Mathematics – C.J TRANTER
    - Pure Mathematics 1 & 2 – Backhouse
    - Mathematics For A level (Volume 1 & 2) – S . Chand
    - Advanced Level Mathematics (Vol 1) – L.K Shayo
9. CHEMISTRY
    - Advanced level physical chemistry with General Chemistry – APE networks 2012, 1st Edition 2011.

- Essential of Physical Chemistry – Arun Bahl
- Organic Chemistry – Arun Bahl, 1st Edition illustrative Reversed 2012

10. ECONOMICS
    - Economic paper one – By ambilikile
    - Economic paper two – By ambilikile
11. ACCOUNTS
    - Bussiness Accounting Volume 1- By Frank Wook
    - Bussiness Accounting Volume 2- By Frank Wook
12. GENERAL STUDIES
    - General Studies for Advanced Level Certificate, Form five – Richard R.F Mbalase
    - General Studies for Advanced Level Certificate, Form six – Richard R.F Mbalase
    - General Studies, supplementary book for advanced and colleges, second edtion – Konrad Adenaker Stiftung

WIZARA YA ELIMU,SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SHULE YA SEKONDARI YA SENGEREMA

FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye Sel Form) …….....
2. Anwani ya nyumbani S.L.P..... WILAYA.....
3. Tarehe ya kuzaliwa ……. .....
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji…….....Kata……...Tarafa……
5. Mahali unapoishi kwa sasa ……..... WILAYA.....
6. Shule ya msingi/Sekondari ulikotokaAnwani……....
7. Dini/Dhehebu…….....Kabila…….....

8. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala yahusuyo shule:

(i) Jina la Baba…… Namba ya Simu …….....
Hai/ Si hai……(kama hai) kazi yake……... Anwani…… (ii) Jina la Mama…….. Namba ya Simu …….....
Hai/ Si hai……(kama hai) kazi yake..... Anwani.....
(iii) Jina la Mlezi ……Uhusiano…… Namba ya Simu .....
Kazi yake……..... Anwani S.L.P..... WILAYA.....

NB. BANDIKA PASSPORT KWENYE VIBOMA ZA WATAJWA HAPO JUU.

passport BABA	**passport MAMA**	**passport MLEZI**

Mimi (Mwanafunzi)…….. nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

…… .....
Sahihi ya Mwanafunzi *Tarehe*

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)…….. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi …… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Sengerema ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanagu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanagu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

…… .....
Sahihi ya Mzazi/Mlezi *Tarehe*

BEI YA BAADHI YA VITU KATIKA DUKA LILILOKO SHULENI

S/No.	***VIFAA***	***BEI***
1.	*GODORO SUPPER BANCO*	*TSH. 40,000*
2.	*GODORO MALAIKA*	*TSH. 25,000*
3.	*SANDUKU LA CHUMA*	*TSH. 24,000*
4.	*SHATI TOMATO*	*TSH. 9,000*
5.	*NETI*	*TSH. 7,000*
6.	*SHUKA NYEPESI*	*TSH. 7,000*
7.	*SHUKA NZITO*	*TSH. 9,000*
8.	*RIM PAPER DOUBLE (AA)*	*TSH. 11,000*
9.	*DUMU LA MAJI LITA 20*	*TSH. 5,000*
10.	*NDOO NDOGO LITA 10*	*TSH. 3,500*
11.	*DUMU LA LITA 5*	*TSH. 1,600*
12.	*TAA*	*TSH. 3,500*
13.	*COUNTER BOOK QIURE 2*	*TSH. 2,500*
14.	*COUNTER BOOK QUIRE 3*	*TSH. 3,500*
15.	*COUNTER BOOK QUIRE 3*	*TSH. 4,000*
16.	*SCIENTIFIC CALCULATOR*	*TSH. 40,000*
17.	*T-SHIRT YA KOLA YENYE NEMBO YA SHULE*	*TSH. 10,000*
18.	*T-SHIRT YA MICHEZO YENYE NEMBO YA SHULE*	*TSH. 5,000*
19.	*TAI YENYE NEMBO YA SHULE*	*TSH. 3,000*
20.	*SWETA LENYE NEMBO YA SHULE*	*TSH. 14,000*
21.	*SURUALI INASHONWA KWA GHARAMA*	*TSH. 14,000*